# STD 6 END TERM 3 EXAM 2019

# KISWAHILI

***Soma kifungu kifuatacho kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo chini. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Uwanja wa michezo __1__ Tononoka ulikuwa umejaa __2__ wa watu. Mashambiki wa timu __3__ mbili walipiga kelele, shangwe na hoihoi. __4__ wa timu yetu __5__ na wachezaji wetu akiwapa ushauri. Timu yetu ilivaa __6__ ya kijani kibichi nayo timu pinzani ilikuwa na nyekundu. Baada ya dakika thelathini na __7__ , timu yetu ilifunga bao la __8__ . Bao hilo lilifungwa na mshambulizi wa timu yetu aliyeitwa Muturi. Muturi alipiga __9__ wachezaji watatu wa timu ile __10__ na kubaki peke yake. __11__ mpira hadi wavuni. Kipindi __12__ pili kilipokaribia kuisha, tulifunga bao la pili. Tuliimba, tukacheza na kuruka kwa furaha. Mara refa alipuliza __13__ kuashiria mwisho wa mchezo. __14__ mashabiki wa timu ile pinzani sana. Je __15__ kama ni wewe ungefanya nini?

| | | | |
|---|---|---|---|
| **1.** A. wa | B. ya | C. la | D. za |
| **2.** A. ukungu | B. mzengwe | C. msongamano | D. umati |
| **3.** A. wote | B. yote | C. zote | D. nyote |
| **4.** A. Koche | B. Kocho | C. Kochi | D. Kocha |
| **5.** A. aliongea | B. aliongelesha | C. alizomewa | D. alikeleleshwa |
| **6.** A. jezi | B. sare | C. nguo | D. fulana |
| **7.** A. minane | B. tano | C. arobaini | D. mitano |
| **8.** A. kuanzisha | B. kuanza | C. kwanza | D. kuanzisha |
| **9.** A. miayo | B. chafya | C. chenga | D. mbizi |
| **10.** A. ingine | B. nyingine | C. zingine | D. mwingine |
| **11.** A. Aliushuti | B. Aliupiga | C. Aliusukuma | D. Aliuburusha |
| **12.** A. ya | B. za | C. vya | D. cha |
| **13.** A. mluzi | B. upepo | C. panda | D. kipenga |
| **14.** A. Tuliwacheka | B. Tuliwachekelea | C. Tuliwachekesha | D. Tuliwachekelewa |
| **15.** A. . | B. ? | C. ! | D. , |

***Kuanzia swali la kumi na 16 hadi 30, jibu kila moja kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Chagua sentensi ambayo **haijatumia kiashiria radidi**.
A. Mkebe uo huo umepewa mtoto.
B. Darasa hili hili lina wanafunzi.
C. Madawati haya haya ni manya

**17.** Jaza pengo kwa jibu sahihi
Mtoto huyu ________ vizuri sana.
A. amelewa
B. amelelea
C. amelelewa
D. amelewea

**18.** Sentensi gani ambayo imetumia alama za mtajo?
A. Ala! Mbona unachezea masomo!
B. Asiyesikia la mkuu….
C. Je, unamjua ng'ombe?
D."Njooni hapa nyote," mama alisema.

**19.** Kutokana na kitenzi funza, tunapata nomino ________.
A. Mwalimu B. Mwanafunzi
C. Fundisha D. Elimu

**20.** Chagua sentensi iliyotumia **'ki'** kuonyesha hali ya udogo.
A. Kikulacho ki nguoni mwako.
B. Ukimwona mwambie asome kwa bidii.
C. Kitoto kilichoanguka kimeumia.
D. Mama alikuwa akipika nilipowasili.

**21.** Kamilisha sentensi kwa jibu sahihi.
Sisi ______ wanafunzi bora shuleni humu.
A. ndio B. ndiyo C. ndisi D. ndiye

**22.** Maumbo haya yanaitwaje?



A. hilali, nusuduara, tao
B. nusuduara, hilali, tao
C. hilali, tao, hilali
D. tao, hilali, nusuduara

**23.** Kiungo gani cha mwili **kisichopatikana** pamoja na viungo vingine?
A. kidaka-tonge B. nyonga
C. paja D. wayo

**24.** Chagua wingi wa: **Udevu wa Musa umeng'oka.**
A. Ndevu za Musa zimeng'oka.
B. Devu za akina Musa zimeng'oka.
C. Ndevu za akina Musa zimeng'oka
D. Devu za Musa zimeng'oka

**25.** Sentensi hii imetumia **'karibu'** kuonyesha nini?
**Mgeni wetu karibu tule chamcha.**
A. maagano B. nusura
C. makaribisho D. umbali

**26.** Chagua jibu la kitendawili hiki: **Dhahabu yangu haishuki bei.**
A. Gari B. Pesa
C. Chakula D. Shamba

**27.** Vifuatavyo ni vyombo vya usafiri vinavyotumika ardhini **isipokuwa**;
A. riksho B. gari la moshi
C. purutangi D. trela

**28.** Jua likiwaka sana bila mvua kunyesha, mimea yote hu________
A. nawiri B. huvunwa
C. stawi D. nyauka

**29.** Kanusha: **Kucheza husaidia mwili.**
A. Kucheza huwa hakusaidii mwili.
B. Kutocheza hakusaidiangi mwili.
C. Kutocheza huwa hakusaidii mwili.
D. Hakucheza wala hakusaidia mwili.

**30.** Chagua orodha iliyo na viunganishi pekee.
A. Lakini, kwa sababu, wala
B. Na, ni, wala, cheza
C. Mtoto, changu, hii
D. Hapa, hapo, pale

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.***

Ugonjwa wa UKIMWI ni kati ya magonjwa mengi ambayo huwaua watu sana kote ulimwenguni. Ugonjwa huu husababishwa na virusi ambavyo hupunguza kinga ya mwili. Kinga ya mwili huwa ni uwezo wa mwili wa binadamu wakupigana na magonjwa. Kinga ikipungua, mwili wa mtu huwa hauwezi ukajilinda dhidi ya magonjwa. Kwa hivyo, mtu aliye na virusi vya UKIMWI huweza kushambuliwa na ugonjwa wakati wowote. Jambo linalofanya ugonjwa huu uwe hatari ni kwa sababu hauna tiba. Hakuna dawa kamili inayoweza kuuponya ugonjwa huu.

Je, ugonjwa huu huwezaje kuingia mwilini? Kuna njia mbalimbali ambazo ugonjwa huu huweza kuingia mwilini. Njia ile inayojulikana sana ni kupitia kushiriki mapenzi na mtu aliye na virusi vya UKIMWI. Hata hivyo, kuna njia nyingine nyingi ambazo huendeleza maambukizi ya UKIMWI. Kwa mfano, mtu akiongezwa damu iliyo na virusi au akitumia vifaa kama vile sindano na wembe pamoja na mwenye virusi unaweza ukaambukizwa ugonjwa huu. Vilevile, mwanamke ambaye ana virusi hizi anaweza kumwambukiza mwanawe asipokuwa mwangalifu.

- Mtu atafanya nini ili asiambukizwe ugonjwa huu? Kwa kuwa ugonjwa huu hauna tiba, **njia ya pekee ni kujikinga**. Ni muhimu sana kujiepusha na mapenzi, kuchunguza damu kabla ya kumwongeza mgonjwa na pia kuwa mwangalifu unapotumia vifaa kama visu, nyembe na sindano.

Ikitokea kuwa mtu ameambukizwa, anashauriwa kuwa **asife moyo.** Bado mtu anaweza akaishi kwa muda mrefu ata akiwa na virusi hivi. Kuna dawa ambazo hupeanwa hosipitalini ili kuwasaidia wagonjwa wa UKIMWI. Mtu akizimeza dawa hizi vizuri, zinaweza zikamsaidia. Isitoshe, anayeugua ugonjwa wa UKIMWI anashauriwa kula vizuri, kufanya mazoezi na kuwacha kuwa na mawazo mengi. Ni vyema sote tuwe makini ili tusipatwe na ugonjwa huu. Aidha, tuwajali na kuwasaidia walioambukizwa.

**31.** Kulingana na aya ya **kwanza** ni kweli kuwa;
- A. UKIMWI ni ugonjwa pekee ambao huwaua watu sana duniani.
- B. Mtu aliye na virusi vya UKIMWI hawezi akashambuliwa na ugonjwa wakati wowote.
- C. Kuna magonjwa mengi ambayo huwaua watu sana ulimwenguni.
- D. Kuna ugonjwa mmoja tu ambao huwaua watu sana ulimwenguni.

**32.** Ugonjwa wa UKIMWI husababishwa na;
- A. Bakteria
- B. Vimelea
- C. Virusi
- D. Vidudu

**33.** Mtu akiambukizwa ugonjwa wa UKIMWI;
- A. Kinga ya mwili hupungua
- B. Kinga ya mwili huondoka
- C. Kinga ya mwili huwa bora
- D. Kinga ya mwili hukosekana

**34.** Ni jambo gani linalofanya ugonjwa wa UKIMWI uwe hatari?
- A. Huwaua watu wengi sana
- B. Dawa yake hupatikana mbali
- C. Hauna tiba kabisa
- D. Hufanya mtu ashambuliwe na magonjwa mengine

**35.** Gani **si** njia ambayo ugonjwa wa UKIMWI unaweza kuingia mwilini?
- A. Kutofanya mapenzi na mtu aliye na virusi
- B. Kuongezwa damu iliyo na virusi
- C. Kutumia vifaa kama sindano na mtu mwenye virusi
- D. Kutoka kwa mzazi mwenye virusi hadi kwa mtoto

**36.** Mwandishi anashauri kuwa njia ya pekee ya kuzuia ugonjwa wa UKIMWI ni kujikinga. Methali gani inayoweza kutumika kuelezea hali hii?
- A. Baada ya dhiki ni faraja
- B. Kifo cha wengi ni harusi
- C. Kinga ni bora kuliko tiba
- D. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki

**37.** Nahau **'asife moyo'** ina maana gani namna ilivyotumiwa katika kifungu?
- A. asiage dunia
- B. asipoteze matumaini
- C. asipoteze roho
- D. asijiue

**38.** Mtu anashauriwa kufanya nini ili asiupate ugonjwa wa UKIMWI?
- A. Kuchunguza maji kabla ya kumwongeza mgonjwa
- B. Kuangalia unapotumia vifaa kama visu, nyembe na sindano
- C. Kujiepusha kabisa na wapenzi
- D. Kuwa mwangalifu unapotumia vifaa kama visu, nyembe na sindano

**39.** Kulingana na kifungu ni kweli kuwa;
- A. Mtu akipata virusi vya UKIMWI, hawezi akaishi tena
- B. Kuna dawa za kumsaidia mgonjwa kufa haraka
- C. Mgonjwa wa UKIMWI anafaa kuwacha kula
- D. Mgonjwa wa UKIMWI anaweza akaishi kwa muda mrefu

**40.** Kifungu hiki kinahusu nini?
- A. Kifo
- B. UKIMWI
- C. Ugonjwa
- D. Afya

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50.***

Katana alizaliwa katika familia ya wazazi waliokuwa wakwasi. Walikuwa na pesa nyingi kama mchanga wa baharini. Baba yake alifanya kazi ya kuendesha ndege. Mama yake naye aliwauguza wagonjwa hosipitalini. **Baba yake Katana alikuwa simba.** Hili lilimsaidia Katana kuwa mwenye bidii sana masomoni. Alisomea katika shule ya Fahari. Shule ya Fahari ilikuwa ya wanafunzi waliotoka katika familia za walalaheri. Wanafunzi wengi katika shule hiyo walikuwa wenye kiburi na majivuno. Wengi hawakupenda masomo. Waliangalia mali ya wazazi wao na kudhani kuwa pia wao walikuwa matajiri.

Hata hivyo, Katana alikuwa tofauti sana na wao. Katana alifahamu kuwa mtegemea cha nduguye hufa masikini. Vilevile, alielewa kuwa mali, magari, runinga na kila kitu kilichokuwa kwao kilikuwa cha wazazi wake bali si chake. **Alisoma kwa bidii kama mchwa**. Wanafunzi wenzake walipochezea tarakilishi na kutazama runinga, Katana alijifungia katika chumba chake na kufanya kazi ya ziada. Baada ya kuzimaliza kazi hizo, alianza kusoma vitabu vya hadithi.

Aliufanya mtihani wa darasa la nane vizuri mno. Akajiunga na shule ya sekondari. Baada ya masomo ya sekondari na chuo kikuu, alipata kazi nzuri yenye mshahara mkubwa. Wale waliokataa kusoma walibaki masikini baada ya wazazi wao **kuaga dunia** na mali kuisha. Wengi wao humfanyia Katana kazi za shambani, kumwoshea magari na hata kumlishia mifugo.

Wewe ungependa kuwa kama Katana au marafiki zake?

**41.** Baba na mama wa Katana walifanya kazi gani?
- A. Udaktari na unesi
- B. Rubani na nesi
- C. Mwalimu na daktari
- D. Rubani na daktari

**42.** '**Baba yake Katana alikuwa simba**' hii ina maana kwamba alikuwa mwenye tabia gani?
- A. Tajiri
- B. Mfalme
- C. Mkali
- D. Mwenye bidii

**43.** Kulingana na aya ya kwanza, ni kweli kuwa;
- A. Kuna wanafunzi katika shule ya Fahari ambao walikuwa wazuri
- B. Wanafunzi wote katika shule ya Fahari walikuwa wabaya
- C. Katana hakusomea katika shule ya Fahari
- D. Shule ya Fahari ilikuwa ya wazazi masikini

**44.** Kifungu kimeeleza kuwa Katana alikuwa mwenye tabia gani?
- A. Mzembe
- B. Mwenye bidii
- C. Mchoyo
- D. Mpenda anasa

**45.** '**Alisoma kwa bidii kama mchwa.**' Maneno haya ni mfano wa__________
- A. tashbihi
- B. istiara
- C. nahau
- D. methali

**46.** Kando na kufanya kazi za ziada, Katana alifanya nini kingine?
- A. Hakutazama runinga
- B. Aliwasaidia wazazi kufanya kazi
- C. Alisoma vitabu vya hadithi
- D. Hakucheza na ndugu zake

**47.** Kiwango cha juu zaidi cha elimu ambacho Katana alifikia ni kipi?
- A. Chuo kikuu
- B. Shule ya upili
- C. Shule ya msingi
- D. Shule ya chekechea

**48.** Baada ya masomo Katana alipata kazi gani?
- A. Udaktari
- B. Udereva
- C. Urubani
- D. Haijatajwa

**49.** Maneno '**kuaga dunia**' yametumika katika aya ya mwisho, ya maana gani?
- A. Kupoteza mali
- B. Kuishiwa na mali
- C. Kufa
- D. Kupoteza kazi

**50.** Kifungu hiki kinatueleza umuhimu wa nini?
- A. Umuhimu wa masomo
- B. Umuhimu wa mali
- C. Umuhimu wa familia
- D. Umuhimu wazazi